**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**MTIHANI WA HISABATI DARASA LA NNE OKTOBA 2024**

| S/N | QUESTIONS | ANSWER |
|---|---|---|
| 1. | i. Andika 700 + 8000 + 60 + 7 kwa maneno | |
| | ii. Andika kwa tarakimu "kumi na tatu elfu mia tatu na shirini na nne" | |
| | iii. Andika XXIX kwa maneno | |
| | iv. Namba zilizopo hapo chini zinaongezeka kwa ngapi? (76,80,84,88,92) | |
| | v. Katika namba 54276, ni tarakimu ipi ambayo inathamani ya 200? | |
| 2. | i. Noti 5 za shilingi 5000 ni sawa na shilingi ngapi? | |
| | ii. Chora na utie kivuli moja ya nne. | |
| | iii. Zipange upya namba zifuatazo kwa kuanza na kubwa kwenda ndogo. 8088,8808,8180,8008,8081. | |
| | iv. Chura aliruka hatua mbili zenye urefu sawa wa sm30. Kama aliruka tena hatua ya tatu yenye urefu sawa na hatua mbili za mwanzo. Ni umbali gani aliruka? | |
| | v. Andika kwa maneno thamani ya tarakimu 7 katika namba ifuatayo 79,083. | |
| 3. | i. Maria alikuwa na mishumaa 6353. Ikiwa mishumaa 3531 ilikuwa mibovu, ni mishumaa mingapi haikuwa mibovu? | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ii. Wanafunzi kumi na mbili wa darasa la nne waligawana pipi arobaini na nane kwa idadi sawa. Je kila mmoja alipata pipi ngapi? | | |
| | iii. Tafuta thamani ya P<br>6 9 7 P<br>+ 3 7 8 3<br>__________<br>_10 7_ 6 0 | | |
| | iv. Nina marumaru 3541 kama nitanunua marumaru 1234 zaidi. Je nitakuwa na marumaru ngapi? | | |
| | v. Andika namba kubwa ambayo inaweza kuundwa kwa tarakimu zifuatazo 3,5,2 na 7 | | |
| 4. | i. Michael hutembea mita 7500 kutoka shuleni hadi nyumbani. Ni mita ngapi atatembea kwenda shuleni na kurudi nyumbani? | | |
| | ii. Saa dakika<br>− 7 25<br>3 35<br>__________<br>__________ | | |
| | iii. Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo<br><br> | | |
| | iv. Ni pembe tatu ngapi unaziona hapo chini?<br> | | |
| | v. Ng’ombe huzalisha lita 25 za maziwa kwa siku. Je atazalisha lita ngapi za maziwa kwa siku 5? | | |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="4">5.</td><td>Ifuatayo ni orodha ya bidhaa pamoja na bei zake katika duka la Bwana Shamba. Soma kwa makini na ujibu maswali yanayofuata.<br><table>
<tr><th>Bidhaa</th><th>Bei</th></tr>
<tr><td>1kg ya unga wa mahindi</td><td>Sh 1200</td></tr>
<tr><td>1lita ya mafuta ya kupikia</td><td>Sh 1200</td></tr>
<tr><td>1pakti ya majani ya chai</td><td>Sh 700</td></tr>
<tr><td>1kg ya sukari</td><td>Sh 2500</td></tr>
<tr><td>1 mche wa sabuni</td><td>Sh 600</td></tr>
<tr><td></td><td></td></tr>
</table></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>i. Ni bidhaa gani ina bei kubwa katika duka la bwana shamba? ____________________</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>ii. Pakti 3 za majani ya chai zitagharimu kiasi gani? _____________________</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>iii. Kilo moja ya unga wa mahindi pamoja na kilo moja ya sukari kwa ujumla zitauzwa shilingi ngapi? _______________________</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="2"></td><td>iv. Ni miche mingapi ya sabuni itagharimu kiasi cha 3600/=? ___________________</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>v. Tafuta tofauti ya bei pakti moja ya majani ya chai na mche mmoja wa sabuni.</td><td></td><td></td></tr>
</table>